

## MLO KAMILI WA KUKU

Kuku site.

Mlo kamili wa kuku ni mlo wenye virutubisho vyote muhimu anavyohitaji kuku kwa kiwango na uwiano sahihi, Virutubisho vinavyohitajika katika mlo wa kuku ni kama ifuatavyo:

### 1.Wanga (carbohydrates)

Wanga hutumika kama chanzo cha haraka cha nishati (nguvu) katika mwili wa kuku, na inapatikana katika nafaka mbalimbali kama Mahindi, Pumba ya mahindi, Ngano, Mtama, Mchele n.k



### 2. Protini ( protein )

Ni kirutubisho muhimu ambacho hujenga mwili. Protini inapatikana katika vyakula kama Mashudu ya Alizeti, Dagaa, Soya, Damu n.k



### 3.Mafuta (Fat)

Mafuta ni muhimu sana katika lishe ya kuku kwani humuwezesha kuku kusharabu fat soluble vitamins kama vitamin A, D, E, na K, huhifadhi nishati, kutunza joto na kulinda ogani muhimu katika mwili wa kuku.

### 4.Vitamini (vitamins)

Ni virutubisho muhimu sana vinavyohitajika kwa kiwango kidogo lakini humfanya kuku awe na afya bora, huzuia magonjwa kama matatizo ya macho, Ulemavu wa miguu n.k



Vitamini hupatikana katika vyakula mbali mbali kama mboga mboga za majani, Nafaka na Matunda. Kuku anayefugwa huria hupata vitamini kutoka katika mazingira anayojitafutia chakula lakini Kuku wanaofugwa ndani hupewa multivitamin ambayo huwa na vitamini zote za msingi na Mara nyingi huchanganywa katika maji ya kunywa.





### 5. Madini (Minerals)

Kuku anahitaji madini kwa ajili ya afya ya mifupa ( Calcium, Phosphorous, Magnesium), Kuweka sawa kiwango cha electrolytes ( Sodium, Potassium na Chlorine) na kwa kiwango kidogo madini kwa ajili ya reactions mbali mbali katika mwili (zinc, manganese, iron, copper, selenium, na iodine). Kuku anayefugwa huria hupata madini kutoka katika mazingira anayojitafutia chakula lakini kuku wa ndani huwekewa premix ambayo huwa na madini ya msingi anayohitaji.



<https://kuku.great-site.net>

### 6. Maji ( Water )

Maji ni muhimu kwa kuku kwani huwawezesha kuku kusharabu virutubisho mwilini na kuwasaidia kuku kupunguza joto la mwili kwa kunywa maji ya baridi katika nyakati za joto.

**MAHITAJI MBALIMBALI YANAYOTUMIKA KATIKA MAANDALIZI YA CHAKULA CHA KUKU PAMOJA NA WASTANI VIWANGO VYA PROTINI GHAFI INAYOWEZA KUMENG'ENYWA (CRUDE DIGESTIBLE PROTEIN).**

MAHITAJI	% Crude protein (CP)
Mahindi	8.5% CP
Ngano	11 - 13.0% CP
Soya	40 - 48% CP
Mashudu ya alizeti	33.9 - 46.8% CP
Damu kavu	80.0% CP
Dagaa	60% CP
Pumba Za mahindi	9 - 12 % CP
Mtama	9 % CP

VIWANGO VYA VIRUTUBISHO MBALIMBALI VINAVYOHITAJIKA KATIKA HATUA ZA UKUAJI WA KUKU:

A. KUKU WA NYAMA ( BROILER)

BROILER	Starter Umri wa kuku Wiki (0- 03 )	Glower Umri wa kuku Wiki (4- 06 )	Finisher Umri wa kuku Wiki (7+ )
Protein ghafi "Crude Protein%" (CP)	22	20	18
Lysine%	1.30	1.15	0.95
Methionine%	0.5	0.45	0.5
Calcium%	0.95	0.90	0.85
Phosphorus%	0.45	0.40	0.35
Fat %	5	5.5	6.0
Fiber %	2.5	2.5	2.5
sodium %	0.18	0.18	0.18
chlorine %	0.18	0.18	0.18

B. KUKU WA MAYAI ( LAYERS)

LAYER	Starter Umri wa kuku Wiki (0- 06)	Glower Umri wa kuku Wiki(07- 18)	Layer Umri wa kuku Wiki (18+ )
Protein ghafi "Crude Protein%" (CP)	20	17	17
Lysine%	1.10	0.80	0.80
Methionine%	0.45	0.35	0.40
Calcium%	1.0	0.95	3.5 - 4.5
Phosphorus%	0.5	0.5	0.35 - 0.5
Fat %	4.0	4.0	4.0
Fiber %	3.0	3.0	3.0 - 4.0
sodium %	0.18	0.18	0.18
chlorine %	0.18	0.18	0.18

Imepakuliwa: 10/09/2024

Inapatikana : <https://kuku.great-site.net>